

Please check the examination details below before entering your candidate information

Candidate surname

Other names

Centre Number

Candidate Number

--	--	--	--	--

--	--	--	--	--

## Pearson Edexcel International GCSE (9–1)

**Friday 2 June 2023**

Morning (Time: 2 hours 15 minutes)

Paper  
reference

**4SW1/01**



### **Swahili**

### **PAPER 1: Reading, Writing and Translation**

**You do not need any other materials.**

Total Marks

#### **Instructions**

- Use **black** ink or ball-point pen.
- **Fill in the boxes** at the top of this page with your name, centre number and candidate number.
- There are **three** sections you must answer:
  - Section A Questions 1–4
  - Section B Questions 5 and **either** Question 6(a) **or** 6(b) **or** 6(c)
  - Section C Question 7.
- Answer the questions in the spaces provided
  - *there may be more space than you need.*
- You must **not** use a dictionary.

#### **Information**

- The total mark for this paper is 80.
- The marks for **each** question are shown in brackets
  - *use this as a guide as to how much time to spend on each question.*

#### **Advice**

- Read each question carefully before you start to answer it.
- Check your answers if you have time at the end.

**Turn over** ►

**P75320A**

©2023 Pearson Education Ltd.  
N:1/1/1/1/1/1/1



**Pearson**

**SECTION A****Reading**

**Answer ALL questions. Write your answers in the spaces provided.**

**Some questions must be answered with a cross in a box . If you change your mind about an answer, put a line through the box  and then mark your new answer with a cross .**

**Open-response questions do not have to be written in full sentences and you may respond using single words or phrases.**

- 1 Malizia sentensi zifuatazo kwa **Kiswahili** na tumia taarifa katika maelezo. Weka alama sahihi kwenye kila kisanduku.

**Kuadhimisha Siku ya Kuzaliwa**

Leo nimepumzika kwangu kwani nimechoka sana. Jana nilikwenda kwenye sherehe ya kuzaliwa ya rafiki yangu na tulicheza dansa na kula vyakula mbalimbali. Baba yake alioka nyama kwenye jiko la mkaa lililokuwa kwenye uwa uliojaa maua. Hakukuwa na viti vya kukalia karibu na jiko hivyo nilisimama huku nikila nyama.

Baadaye rafiki yangu alikata keki na kuwalisha watu kwa uma. Mimi niliona ukosefu wa usalama kulishwa kwa uma uliotumiwa na wengine hivyo niliweka keki kwenye kiganja changu. Pia tulitunukiwa vitu tofauti na mwenyeji ingawa kwa kawaida wageni huleta chocote.

Mama yangu alitakiwa anifuate lakini msongamano wa magari ulinilazimisha kutembea karibu kilometra sita. Bahati nilikuwa na rafiki zangu na tulizungumza njiani.



- |                     |                   |                            |                       |
|---------------------|-------------------|----------------------------|-----------------------|
| <b>A</b> karamuni   | <b>B</b> hatari   | <b>C</b> kelele            | <b>D</b> mapochopocho |
| <b>E</b> zawadi     | <b>F</b> salama   | <b>G</b> bustani           | <b>H</b> vitini       |
| <b>I</b> mazungumzo | <b>J</b> nyumbani | <b>K</b> <del>uchovu</del> | <b>L</b> foleni       |
| <b>M</b> bure       |                   |                            |                       |

<b>Example:</b>	Sababu ya kupumzika ...	<b>K</b>
1 (a)	Mahali anapopumzika ni ...	
1 (b)	... mengi yaliliwa karamuni	
1 (c)	Nyama ilichomwa katika ...	
1 (d)	Kutumia uma mmoja kwa wote ni ...	
1 (e)	Kinyume na mazoea wote walipewa ...	
1 (f)	Alitembea sana kwa sababu ya ...	


**(Total for Question 1 = 6 marks)**



- 2** Weka alama katika visanduku **10** vilivyo sahihi. Sentensi nyingine au watu wengine wanaweza kuwa na alama zaidi ya moja au bila alama yoyote.

### Shuleni

#### Asha



Shuleni kwetu tunavaa sare nyeusi na haturuhusiwi kusuka nywele. Wazo la kuvaasare ni zuri, ingawa ningefurahia kama rangi ingekuwa tofauti. Sichelewi kufika shuleni kwani sina bughudha ya kuchagua nguo asubuhi na hakuna ruhusa ya kujipoodoa jambo linalonisaidia kutopoteza muda.

#### Sabrina



Ninapofanya mazoezi shuleni, ni lazima nibebe sare zetu za rangi nyekundu ambazo ni nzito na hunitoa jasho. Mimi hubadili kabla ya mazoezi kwani huzibeba mfukoni. Watu wanasema zinanipendeza sana. Lakini kawaida tunapoenda shuleni sisi huvaan nguo za nyumbani na hujipoodoa. Mimi huchagua nguo usiku kwani sipendi kuchelewa.

#### Hirsi



Ningefurahi kama tusingekuwa na sare za shule. Sare yetu ni rangi nyeupe kwa hivyo huchafuka kirahisi mno. Pia tunavaa koti linalonitoa jasho. Ninachukia kufua sare zangu hivyo mimi hubeba nguo za nyumbani na hubadilisha ninapotoka shule ingawa hii huniongezea bughudha.

		Asha	Sabrina	Hirsi
<b>Mfano:</b>	Haruhusiwi kusuka	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
<b>A</b>	Hubadili sare anapokuwa shulenii	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
<b>B</b>	Hafurahii kuwa na sare	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
<b>C</b>	Angependa rangi ya sare ingebadilika	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
<b>D</b>	Shule inaruhusu kujipodoa	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
<b>E</b>	Anajitahidi asichelewe	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
<b>F</b>	Sare humpa joto mwilini	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>

(Total for Question 2 = 10 marks)



P 7 5 3 2 0 A 0 5 1 6

- 3** Soma makala kuhusu likizo kijijini. Malizia taarifa kwa kutumia namba au maneno kwa **Kiswahili**.

### **Likizo Kijijini**

Ninaitwa Juma. Likizo iliyopita nilienda Msumbiji kumtembelea rafiki yangu. Nilizungumza naye mara kwa mara kabla ya kumwuliza kama ningeweza kumtembelea. Ndege yetu ilichelewa lakini nilishukuru nilipowasili uwanjani na kumkuta rafiki yangu akinisubiri. Akaniambia alihamia kijijini kwa hivyo tutaenda huko. Nilikuwa na hamu ya kuenda ingawa gari letu liliharibika tulipokuwa njiani.

Tulipofika kijijini kila mtu alitukaribisha kwa vigelegele. Nilipewa mihogo ya kuchemsha na pilipili. Nilipoanza kula ikatokea kelele kali kutoka nje. Sote tukasimama na kukimbilia nje kuona nini kilikuwa kinaendelea. Huko tulimkuta mtoto wa jirani amelala kifudifudi. Tulipomkaribia alisimama na kuanza kucheka. Kumbe ilikuwa ni mchezo wa watoto kutaka kutushtua. Sote tulifyonza na kuondoka.

Nilirudi ndani ili kumalizia chakula changu. Ilipofika jioni tulienda kuzunguka kijijini. Nyumba nyingi zilikuwa za mviringo. Tulitembea hadi kwenye mpaka wa kijiji ambapo kulikuwa na msitu na nilivutiwa kuwaona kuku na vifaranga.



**Mfano:** Nchi aliyotembelea: ..... **Msumbiji**

- (a) Mtu aliyetembelewa: ..... (1)
- (b) Nani alitoa wazo la safari: ..... (1)
- (c) Aina za usafiri zilizotumiwa: ..... na  
..... (2)
- (d) Namna alivyopokelewa kijijini: ..... na  
..... (2)
- (e) vitendo alivyofanya mtoto ..... na  
..... (2)
- (f) Hisia yake kuhusu mchezo wa watoto ..... (1)
- (g) Muundo wa nyumba : ..... (1)
- (h) Ukingoni mwa Kijiji kuna ..... na  
..... (2)

**(Total for Question 3 = 12 marks)**



- 4 Soma habari ifuatayo kutoka kitabu kitiwacho **Mwendawazimu na Hadithi Nyingine**, kilichohaririwa na Mwenda Mbatiah na kuandikwa na Ken Walibora**

### Kipara-Ngoto

Jioni moja baba alituambia, "ndugu yangu amemdekeza mtoto wake na kumharibu, ninataka aje hapa ili tumrekebishe." Baada tu ya tangazo hilo mama alibadilika. Lililonifanya nigundue kuwa amekereka ni vita baridi aliyompiga baba kwa siku nyingi baada ya hapo. Mama alijiinamia kama kondoo na alipoulizwa lolote na baba, jibu lake likuwa jicho la hasama. Baba hakusema kitu.

Pamoja na umri wangu mdogo, nilibaini pamepita hitilafu katika mahusiano ya wazazi wangu. Na kisa ni Matata. Wazo hili lilinipa changamoto kwani nyumba yetu ilipoteza furaha kabla hata Matata hajawasili kwetu.

Matata aliingia kwetu wiki mbili baada ya tangazo la baba. Nilimkagua kama mnunuzi akaguavyo ng'ombe mnadani. Alikuwa kijana mwenye takriban miaka 17. Nafikiri alivaa viatu saizi 13 kwani miguu ilikuwa mirefu kupita kiasi.

Mama alimpokea shingo upande na wakawa na mchezo wa paka na panya. Kweli, akufukuzaye hakuambii toka. Hata Matata alipojipweteka kochini na kujidai anasoma kitabu, mama hakudanganyika na alimwangalia kwa ufahamu kuwa ule ulikuwa ulaghai tu.

Jibu maswali kwa **Kiswahili** na tumia taarifa katika maeleo. Si lazima kuandika sentensi kamili.

- (a) Baba anasema mtoto ana shida gani?

Taja maeleo **mawili**

(2)

- (b) Matendo gani yanaonyesha kuna vita baridi kati ya mama na baba?

Taja maeleo **mawili**

(2)



(c) Kwa nini mwandishi hampendi Matata?

Taja maelezo **mawili**

(2)

(d) Matata alipokelewa vipi na mwandishi.

(1)

(e) Mwandishi anakielezeaje kiwiliwili cha Matata?

(1)

(f) Tunagunduaje uhusiano kati ya mama na Matata?

Taja maelezo **mawili**

(2)

**(Total for Question 4 = 10 marks)**

**TOTAL FOR SECTION A = 38 MARKS**



P 7 5 3 2 0 A 0 9 1 6

**SECTION B****Writing**

**Answer Questions 5 and either Question 6(a) or 6(b) or 6(c).**

**Write your answers in the spaces provided.**

**5**

**Lugha**

Lugha unayozungumza nyumbani

Vitabu upendavyo vya utotoni

Lugha ya kufundishia

Lugha wakati ujao

Andika takriban maneno 70 kwa **Kiswahili** kuhusu lugha. Ni lazima kutumia maneno yote yaliyotajwa hapo juu.

(12)



**DO NOT WRITE IN THIS AREA**

**DO NOT WRITE IN THIS AREA**

**DO NOT WRITE IN THIS AREA**

**(Total for Question 5 = 12 marks)**




P 7 5 3 2 0 A 0 1 1 1 6

- 6 Chagua **moja** kati ya maswali matatu yafuatayo na andika takriban maneno 130 kwa **Kiswahili**.

### Chaguo 1

(a)



Andika hotuba kuhusu bustani za umma. Ni lazima uandike kuhusu:

- Umuhimu wa kuwepo bustani za umma
- Kumbukumbu katika bustani uipendayo
- Baadaye bustani zitakuwaje

(20)

### Chaguo 2

(b)

Mpendwa Hannah

*Juzi nilinunua nguo mtandaoni. Bado ninasubiri vitu nilivyonunua viletwe nyumbani.  
Ninajuliza kama vitakuwa kama kwenye picha za mitandaoni au la.*

Nitakuarifu

Rafikiyo,

Aaliyah

Jibu kwa kutumia barua pepe. Ni lazima uandike kuhusu:

- Kumbukumbu ya kununua dukani
- Mawazo yako kuhusu ununuzi mtandaoni
- Ununuzi utakuwaje miaka ijayo

(20)



**Chaguo 3**

(c) Kwenye ukurasa wako wa blogu andika kuhusu usafiri. Ni lazima uandike kuhusu:

- Usafiri uupendao
- Mawazo yako kuhusu usafiri wa umma
- Usafiri utakavyokuwa miaka ijayo

(20)

**Indicate which question you are answering by marking a cross in the box . If you change your mind, put a line through the box  and then indicate your new question with a cross .**

Chosen question number: **Question 6(a)**  **Question 6(b)**

**Question 6(c)**



P 7 5 3 2 0 A 0 1 3 1 6



**DO NOT WRITE IN THIS AREA**

**DO NOT WRITE IN THIS AREA**

**(Total for Question 6 = 20 marks)**

**TOTAL FOR SECTION B = 32 MARKS**



**SECTION C****Translation into Swahili****Write your answer in the space provided.**

- 7 Tafsiri aya ifuatayo kwa **Kiswahili**.

**Abdulrazak Gurnah**

Abdulrazak Gurnah has been awarded the 2021 Nobel Prize for Literature. He received £840,000 for winning this prize. Gurnah who is 73 has authored 10 novels. His novel titled *Paradise* has been translated into Swahili.

Gurnah who lives in England and travels to East Africa whenever he can, couldn't believe he had won when he first heard the news of the award. He thought someone was joking. The award has made him very happy. He says that writing is not about one thing but it is about the things that concern human life.

---

**(Total for Question 7 = 10 marks)**

---

**TOTAL FOR SECTION C = 10 MARKS**  
**TOTAL FOR PAPER = 80 MARKS**

**DO NOT WRITE IN THIS AREA**

**DO NOT WRITE IN THIS AREA**

## **BLANK PAGE**

### **Source Information**

#### **Question 2**

- © SDI Productions/Getty Images
- © Getty Images
- © valentinrussianov/Getty Images

#### **Question 6**

- © ilyaliren/Getty Images

